



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA WANACHAMA WA NHIF KUHUSU UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU BAADA YA KUENZA UTEKELEZAJI WA KITITA CHA MAFAO CHA MWAKA 2023

1 Machi, 2024, Dar es Salaam

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeona matangazo ya kusitisha huduma kwa wanachama wa NHIF kwa baadhi ya vituo binafsi ambavyo ni Regency Medical Center, Kairuki, Hospitali za TMJ, Hospitali ya Apollo na Hospitali zote za Aga Khan nchini kuanzia tarehe 1 Machi, 2024 kinyume na mkataba wa utoaji wa huduma baina yake na NHIF ambao pamoja na mambo mengine unamtaka mtoa huduma kutoa notisi ya siku 90 kabla ya kusitisha huduma.

Kwa tangazo hili, ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza, Mfuko unawatangazia wanachama wake:-

- **Kutumia vituo mbadala** ili kupata huduma wanazohitaji.
- **Maofisa wa NHIF watakuwa katika vituo** kuhakikisha wanachama wenye changamoto wanasaidiwa kupata huduma katika vituo vingine.
- **Mfuko umeshaanza kuwasiliana na wanachama** wenye matibabu yanayohitaji mwendelezo wa huduma ikiwemo huduma za kuchuja damu (dialysis) ili kuwaelekeza vituo mbadala kwa ajili ya upatikanaji wa huduma hizo.

Vile vile, **Mfuko unaendelea kufanya usajili wa vituo vingine binafsi ili kuongeza wigo wa watoa huduma na kusogeza huduma kwa wanachama.** Aidha, Mfuko utaendelea kutoa taarifa ya upatikanaji wa huduma ili kuondoa usumbufu.

Mwanachama asisite kuwasiliana na NHIF kupitia namba ya bure ya **Huduma kwa Wateja 199** endapo atahitaji maelezo zaidi.

Imetolewa na;


Anjela Mziray
MENEJA UHUSIANO

Jengo la NHIF Tambukareli, Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P 1437, Dodoma, Simu: +255 26 2 963 888,
Barua pepe: info@nhif.or.tz, Tovuti: www.nhif.or.tz